

Kufanya uchaguzi kwa Miaka ya shule ya 11 na 12

Taarifa kwa wazazi na walezi

Wanafunzi wanaweza kupendezwa kusoma masomo ya chuo kikuu, kuwa na taaluma maalum akilini ambayo itahusisha elimu na mafunzo zaidi, au kunuia kuingia kazini baada ya kumaliza shule. Kuna chaguzi nyingi kwa wanafunzi katika Miaka 11 na 12 ambayo hutoa njia nyingi za chuo kikuu, mafunzo na ajira.

Chaguzi za kozi na programu kwa Wanafunzi wa Mwaka wa 11 na 12.

Chaguzi	Maelezo
Kozi za ATAR	Kozi za Kiwango cha Uandikishaji cha Juu cha Australia (ATAR) kwa kawaida huwa na mwelekeo wa kitaaluma. Wanafunzi wanaotaka kufikia ATAR wanapaswa kukamilisha kiwango cha chini cha kozi nne za ATAR mwaka wa 12 wa masomo. Ingawa kwa kawaida hufanywa ili kupata masomo ya chuo kikuu, kozi za ATAR pia ni maandalizi bora kwa ajili ya njia mbalimbali za baada ya shule, pamoja na mafunzo ya ufundi.
Kozi za Jumla	Kozi hizi kimsingi zinawalenga wanafunzi ambao kwa kawaida wana nia ya kuingia katika mafunzo ya juu zaidi ya ufundi stadi au kuingia kazini baada ya kumaliza shule. Kozi za jumla hazina mitihani ya nje kama vile kozi za ATAR, lakini zina kazi ya lazima iliyowekwa nje katika Mwaka wa shule wa 12 yenye thamani ya asilimia 15 ya tathmini ya jumla ya mwanafunzi. Wanafunzi wanaweza kutumia baadhi ya kozi za jumla kama sehemu ya njia mbadala ya kuingia katika baadhi ya kozi za chuo kikuu.
Kozi za Msingi	Zimeundwa kwa ajili ya wanafunzi wanaohitaji usaidizi ili kufikia viwango vya chini zaidi vya kusoma na kuandika na/au kuhesabu kabla ya mwisho wa Mwaka wa shule wa 12. Kozi hizi hutoa mkazo katika ujuzi tendaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu, uzoefu wa vitendo unaohusiana na kazi na fursa ya kujenga ujuzi binafsi ambao ni muhimu kwa maisha na kazi. Kozi za msingi hazina mitihani, zina jukumu la lazima lililowekwa nje katika Mwaka wa 12 ambalo lina thamani ya asilimia 15 ya tathmini ya msingi ya shule ya mwanafunzi kwa kozi hiyo.
Hitimu za VET	Wanafunzi hukamilisha sifa ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi inayotambulika kitaifa (VET). VET hujenga ujuzi na maarifa kazini na mahali pa kazi. Wanafunzi wanaweza kutumia sifa za VET kuhesabu Cheti cha Elimu cha Australia ya Magharibi (WACE).

Programu zilizoidhinishwa	Programu zilizoidhinishwa hutoa mafunzo kupitia shughuli ambazo hazijashughulikiwa na kozi za WACE au programu za VET. Programu zilizoidhinishwa ni za wanafunzi wanaotaka kushiriki katika programu ambazo hutolewa katika mazingira mbalimbali na shule, mahali pa kazi, vyo vikiu na mashirika ya jamii. Programu zilizoidhinishwa zinaweza kutolewa kama sehemu ya mtaala wa shule au kama shughuli za ziada za mitaala na wanafunzi wanaweza kuzitumia kuhesabu kuelekea WACE.
Kozi za awali	Kozi za awali zimeundwa kwa ajili ya wanafunzi ambao wametambuliwa kuwa na ugumu wa kujifunza na/au ulemavu wa kiakili. Kozi hizi hutoa chaguo kwa wanafunzi ambao hawawezi kufikia ATAR, maudhui ya kozi ya jumla au msingi na marekebisho na/au masharti ya ulemavu. Vitengo vya awali havichangii katika kufanikisha WACE.